REPUBLIC OF KENYA

COUNTY ASSEMBLY OF KILIFI

THIRD ASSEMBLY-THIRD SESSION

THE HANSARD

Tuesday, 5th March 2024

The House met at the County Assembly Chamber,
Malindi Town, at 9:30 a.m.

[The Temporary Speaker (Hon. Stephen) in the Chair]

PAPER LAID

THE COUNTY FISCAL STRATEGY PAPER, 2024

The Leader of Majority (Hon. Ibrahim): Thank you, Mr. Speaker. I beg to lay the following Paper on the Table: -

The County Fiscal Strategy Paper, 2024. Thank you, Mr. Speaker, Sir.

(Hon. Ibrahim laid the document on the Table)

The Temporary Speaker (Hon. Stephen): Hon. Members, the tabling of the County Fiscal Strategy Paper, 2024 stands committed to all Sectoral Committees who will compile a Report and submit it to the Budget Committee. Thank you. Next Order!

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

MOTION

THANKS FOR THE SECOND SENATORIAL ADDRESS – THIRD ASSEMBLY 2024

The Leader of Majority (Hon. Ibrahim): Thank you, Mr. Speaker, Sir. I beg to move the following Motion: -

> THAT, the thanks of the County Assembly be recorded for the exposition of public policy contained in the Address of the Senator (Rtd) Justice Steward Madzayo CBS, given on Thursday 22nd February 2024.

Thank you, Mr. Speaker.

The Temporary Speaker (Hon. Stephen): Hon. Members, on Thursday, 22nd February 2024 the Hon. (Rtd.) Justice Steward Madzayo CBS graced the House and gave his Second Address. According to the Standing Orders, the Senator's Address was tabled, and a Notice of Motion was given to record the County Assembly's gratitude for the public policy exposition in the Address. Copies of the same were availed to Members' pigeonholes. The debate on this Address will be limited to three sittings starting today. The Address was tabled on Monday, 4th March 2024.

(Question proposed)

The Leader of Majority (Hon. Ibrahim): Asante, Bw. Spika, kwa kunipatia nafasi hii kuchambua hii *speech* ya Seneta wetu wa Jimbo la Kilifi.

Kwanza, ningeomba kupongeza Spika wetu wa Jimbo la Kilifi; nimeona amechaguliwa kuwa Spika bora Kenya nzima lakini hapo kwa kuchaguliwa kama Spika bora ni furaha kwetu sisi lakini nina dukuduku kwamba je, amechaguliwa kwa madhumuni gani? Sasa ningependa wewe pia kwa sababu uko katika *Speakers' Panel*, je una ufahamu ya kwamba amechaguliwa Spika bora ili nipate kuendelea katika hotuba ya Seneta, naomba ufafanuzi kwako pengine una ufahamu ndio amechaguliwa kama Spika bora…nafikiri umenifahamu?

The Temporary Speaker (Hon. Stephen): Eeh nimekufahamu.

(Laughter)

Asante mheshimiwa *Leader of Majority* kwa kuuliza swali hilo. Kwa leo, wacha tuzungumzie hii Hotuba ya Seneta wetu lakini hilo swala ambalo ameliuliza nitalifanyia uchunguzi kidogo halafu nitakuletea majibu wakati mwengine.

The Leader of Majority (Hon. Ibrahim): Asante, Bw. Spika. Nasimama hapa kuchambua Hotuba ya Seneta wetu. Bunge hili liko kisheria na sisi kama wajumbe tuko na nidhamu yake kama Bunge na ukiangalia hotuba ya Seneta wetu aliangazia kwamba kulingana na sheria kifungu nambari 253(1) inamruhusu yeye kuja kuhutubia Bunge letu la Kilifi kwa mujibu wa sheria. Tunaungana naye barabara lakini tukumbuke Bunge hili ni Bunge la heshima na nidhamu.

Japo kuwa katiba na sheria inakubali Seneta kuja kuhutubia Bunge lakini anatakikana pia aheshimu Bunge hili. Si vyema kutumia uongo katika hotuba yake ambapo niko na ushahidi wa kutosha katika Bunge hili. Ndani ya hotuba yake aliangazia akasema ya kwamba upande wa *County Public Service Board* ukabila umekithiri na dhuluma.

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Bw. Spika, *County Public Service Board* ikiongozwa na Mheshimiwa Zia bado ile Bodi ni mpya na kutoka iapishwe na imeajiri watu tisa peke yake. Haijaajiri zaidi ya watu tisa. Naweza nikatoa ufahamu ya kwamba katika watu hao waliojariwa na *County Public Service Board* ni manispaa Meneja watatu, *Engineer* wawili, *Town Planner* wawili, *Director of Disaster* mmoja na mmoja ni *Director* wa Wezesha *Fund*. Katika watu hawa tisa mtaita ni mmoja, mgiriama ni mmoja, msomali mmoja, mjaluo mmoja, mrabai mmoja, jamii ya Kiswahili mmoja, mkikuyu mmoja na wachonyi wawili. Ukabila uko wapi?

Bw. Spika, wakati ukipewa nafasi kuja kuhutubia, si yeye wala Gavana ni muhimu waje watoe maelezo barabara kwa sababu ukisema *County Public Service Board* hapa tuko na *Chairman*, Seneta hakujaribu kukaa na *Chairman* kumuelezea kuna makosa fulani na fulani. Ukija ukisema Bodi unafanya makosa kudhalilishi serikali, unadhalilisha Bunge hili kwa sababu tunaongozwa na mwenyekiti hapa.

Bw. Spika, ukiangalia tena Hotuba yake iliangazia kuhusu mambo ya *tender*; akaongelea mambo ya ufisadi. Si vyema kwa sababu kitengo cha *anti-corruption* kiliingilia kati kuhusiana na mambo ya *tender* ya *revenue collection*. Ndani ya serikali yetu hakuna mtu yeyote aliyeshikwa; hakuna mtu yeyote aliyeandikisha *statement*, hakuna mtu yeyote aliyehojiwa kuhusu mambo ya *corruption*. Si vyema leo uje katika Bunge hili useme ya kwamba *corruption* imekithiri katika jimbo letu. Ni kuvua nguo serikali yetu, ni kuvua nguo Bunge letu. Hatukatai kama kuna ufisadi uko na uhuru wa kuongea lakini zungumzia kitu cha ukweli na usawa ili na sisi tuweze kusaidia.

Pia aligusia mambo ya elimu; katika Kaunti 47, sisi ndio kaunti pekee tumeweza kupeleka watoto *national schools* zaidi ya watoto 2,800. Anazungumzia ya kwamba katika elimu kuna *corruption*, ni *corruption* gani? Alikuwa awe wazi kama kuna fedha zimepotea na kama kuna mtu anahusika. La kushangaza zaidi, wiki iliyopita Gavana na Waziri wetu wa Fedha na Waziri wa Elimu waliitwa *Senate* na tunashukuru ya kwamba walipofika kule waliambiwa wao wako weupe kama pamba. Sasa huku unaongea hivi na wewe ni Seneta na maseneta wenzako ambao wanahusika kukagua mipangilio ya kaunti wanaongea hivi.

Bw. Spika, mimi nilikuwa nataka kusema hivi; hatutoruhusu tena mtu aje hapa kuongea mambo ya siasa; hili si Bunge la siasa hili ni Bunge la sheria na ni Bunge la heshima. Ikiwa Seneta atakuja hapa, mimi ninaongea kama Kiongozi wa walio Wengi, hatutampatia nafasi ya kuongea maneno kama haya ambayo ameongea; si heshima kwetu sisi kama serikali. Aliongezea pia akapongeza; huku ametugonga, huku anapongeza Kitengo cha Afya. Sisi kama serikali ya Jimbo la Kilifi, katika Kaunti 47 tumekuwa namba kumi kuhusiana na mambo ya afya. Katika Pwani tumekuwa namba moja.

Alikuwa apongeze yeye kwa mara ya kwanza kwa miaka 15 yake hakujawahi fanyika kitu kama hicho, alikuwa ajipongeze yeye mwenyewe, lakini ukiangalia hii hotuba yake nyingi sana anagusia urongo; anagusia siasa na hiyo si heshima katika hili Bunge. Na pia vile vile, la kushangaza ni kwamba ni Seneta wangu wa Azimio, anakuja kuponda serikali ya Azimio ndani ya Bunge. Haijawai fanyika, madhimuni yake sijui ni nini na sijui alikua anataka nini. Kwa hivyo, kwa hayo machache nasema kwamba nimekashifu hotuba ya Seneta Madzayo; ni Hotuba ya kiupuzi, ni hotuba ya kijinga na ni hotuba ambayo haina mwelekeo wowote.

Asante sana, Bw. Spika.

The Temporary Spika (Hon. Stephen): Asante sana, kwa mchango wako Kiongozi wa Walio wengi. Waheshimiwa, bado tunaendelea na majadiliano. Mheshimiwa Hassan.

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. Hassan: Asante, ndugu yangu Spika. Kwanza, nashukuru kwa kupewa hii nafasi. Mimi kabla sijaenda mbali, kwanza nataka kurudia hapa alipozungumza ndugu Senata kuhusu maswala ya elimu. Ametukashifu kwamba elimu inazidi kudorora. Kwa bahati nzuri ama bahati mbaya huyu mtu tumekuwa na yeye kama Seneta wetu kwa kipindi cha miaka kumi, huu ukiwa ni wa kumi na moja. Sijui ni lini aliwahi kuitisha kongamano la walimu au wanafunzi ikiwa yeye ni mmoja katika wale washikadau wa Kilifi na mmoja katika wasomi wa Kilifi.

Yeye binafsi kama Seneta, amejitahidi vipi kabla akashifu watu wengine? Kwa hivyo, nataka kusema huyu bwana ni mzembe ambaye hajielewi na hajitambui. Akiwa siku nyingine hana la kuzungumza ama nitasema hivi, hotuba zake kabla hazijafika ndani ya hili Bunge twaomba tuzipitie ndio tumruhusu aingie hapa ndani.

Nikinukuu hapa katika hii hotuba yake anasema Seneti inawakilisha kaunti na kutumikia na kulinda masilahi ya kaunti ya serikali zao. Bunge la Kwanza la Kaunti nilikuwa hapa mshahara tulikuwa tukilipwa laki tatu na alfu sitini (Kshs360,000), Bunge la Pili pia nilipata bahati nikawa niko hapa, tulikuwa tukilipwa pesa zilipunguwa zikaja laki moja na elfu sitini na tano (Kshs165,000), Bunge la Tatu pia nimebahatika niko hapa, saa hii twalipwa shilingi elfu themanini (Kshs80,000). Huyu ametutetea maslahi yetu vipi? Kwa sababu huko kwao wao mishahara inazidi kuongezeka lakini sisi hapa kwetu hakuna chochote. Leo sisi mpaka pesa za kwenda kukaa vikao bado ni matatizo, anatusaidia vipi huyu? Na anasema wao ndio wanatushughulikia sisi pamoja na masilahi yetu huyu hatushughulikii sisi anashughulikia tumbo lake, sio sisi. Na ni vibaya sana mtu mzima kama huyu kuzungumza maneno ya urongo kama haya.

Amezungumza hapa kwamba Kilifi kuna raslimali nyingi lakini sasa zinahitaji… *okay fine,* yeye ameleta *investor* gani katika kujitahidi kwamba Kilifi iwe bora kiuchumi? Kwa sababu unajua wakati unatoa kashfa ni uwe na suluhisho. Ni lini ashawai kuleta *investor* kwa Kaunti yake ya Kilifi pengine?

Mimi nashindwa, mheshimiwa Spika, akija akitoa kashfa hizi za kusema kwamba usimamizi si mzuri sijui *Public Finance,* mimi simuelewi huyu mtu. Sijui ni ule utu uzima… nawaomba waheshimiwa 2027 mnichague kama Seneta…

(Laughter)

Amezungumzia swala la usimamizi wa mfuko kufanya *oversight*. Hizi pesa za uwezo sijui Wezesha *Fund*, hizi pesa nafikiri zinatuhusu sisi waheshimiwa. Haijahusu Seneti na wale wanaochukua hizi pesa ni watu wetu sisi, yeye bado hazijamhusu mbona yuko *very much interested* na hizi pesa lakini masilahi yetu sisi binafsi hako *interested* nayo leo mbunge aki *serve term* mbili hata yeye ame *serve* zaidi ya moja akitoka atakuwa anaendelea kulipwa mshahara wake na bado kuna marupurupu anapata wewe hapa hata uka *serve term* kumi ukitoka umetoka wewe peke yako na hakuna chochote kitakachokufuata kule nyuma. Hebu kama ni kweli yeye ni mtetezi wetu atufanyie haya ndio tutamtambua lakini kwa sasa mimi sijamtambua kama yeye ni mchapa kazi. Asante.

The Temporary Spika (Hon. Stephen): Asante sana, mheshimiwa kwa mchango. Mheshimiwa Grace.

Hon. (Ms.) Grace: Asante, Bw. Spika, kwa kunipatia fursa hii. Nimechambua hii hotuba ya Seneta, hii ni hotuba ya pili kutoka niingie hili Bunge na inasikitisha sana kila wakati Bw. Seneta akija hapa yeye kama muwakilishi katika Bunge la Seneti kwa elimu ambayo niko nayo,

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

anafaa kuja hapa atuelezee ni pesa ngapi serikali iliyopita iliwacha, ni pesa ngapi ameongeza, ni pesa ngapi zimetumika, ni miradi ipi ambayo iliwekwa na ikatengewa pesa kiwango fulani na miradi ipi ambayo haijafanyika lakini pesa zilitumika. Yeye ndio macho yetu lakini katika hotuba zake mbili nimeziona kutoka niingie katika hili Bunge ni siasa. Akija hapa aanze kutuambia mambo sijui Ruto amefanya, Ruto amefanya lakini yeye kama macho yetu anasaidia vipi hii Kaunti?

Alikuja hapa akatuelezea kuhusu mambo ya Shakahola, akawa anasema sijui serikali sijui Ruto sijui nini. Nadhani hapa Kilifi Kaunti kuna Wizara ya Afya na ile Wizara ya Afya inajua ni mikakati ipi ambayo imetumika na Serikali Kuu ikishirikiana na Serikali ya Kaunti. Mipangilio iko, kuna uchunguzi unaendelea lakini Bw. Seneta hakuja hapa kutuelezea ule uchunguzi unaendelea na umefikia wapi; yeye akija hapa ni siasa ni siasa na ni siasa. Hili Bunge lazima liheshimiwe na ninalaumu sana waliozunguka na yeye wakisema arudi hiki kipindi maana walitukosea sana sisi wana Kilifi.

Maseneta wengine kule kwao wanang'ang'ana Kaunti zao ziongezwe pesa. Jana niliona pahali *most of the counties* zimeongezwa pesa lakini nilitafuta jina la Kilifi nikakosa. Wakati mwengine, Bw. Spika, ninaomba kama Seneta atakuja hapa aanze kusema mambo ya siasa tutatoka nje, atabaki na hili Bunge.

Pili, inasikitisha Seneta aje hapa aanze kuzungumzia mambo ya elimu na hata kipofu aliona vile pesa ziligawanywa. Inasikitisha sana na ni aibu huyu Seneta sijui kama yuko Kilifi ama yuko nje ya nchi sielewi. Kwa hivyo, huyu ametuaibisha na akija hapa *next time* asije akatuambia serikali imefanya; yeye ndiye ametumwa aende kule atuwakilishe wala siyo kuja hapa kuanza kutuambia…

(Hon. Changawa stood on a Point of Order)

The Temporary Speaker (Hon. Stephen): Mheshimiwa Grace, kuna malalamishi kidogo kutoka kwa mheshimiwa wa Dabaso, tafadhali *go ahead*.

Hon. Changawa: Asante, mheshimiwa Spika. Mnenaji ambaye yuko kwa Sakafu amesema hata kipofu ameona, sasa tunataka aeleze vizuri maana tunajua kipofu ni nani na kuona haoni. Asante.

(Laughter)

The Temporary Speaker (Hon. Stephen): Haya, nafikiri mheshimiwa Grace jaribu kufafanua hapo maana umeelewa mheshimiwa ni kama kipofu haoni, lakini wewe umesema hata kipofu aliona, labda ufafanue kidogo.

Hon. (Ms.) Grace: Asante, Bw. Spika. Kumanisha 'kipofu'a ulikuwa ni msemo, nilikuwa namaanisha kila mtu aliona na alisikia. Hata huyo kipofu, alisikia. Nafikiri nimeeleweka.

The Temporary Speaker (Hon. Stephen): Asante. Nafikiri mheshimiwa umekubali hapo. Endelea, mheshimiwa Grace.

Hon. (Ms.) Grace: Nasema Senata akija hapa asihutubie ni kama anahutubia wana siasa, siasa tunaziacha kule nje, hapa ni kazi. Asije hapa akaanza kutupatia malalamishi, sisi kazi yetu tunaifanya, kwa kimombo kazi yetu ni *Oversight* hapa *Kilifi County*. Kazi yake, ni afanye huko Seneti. Mambo ya kutuletea siasa, asituletee siasa hapa.

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Kama ni mambo ya miili ya Shakahola afuate Wizara ya Afya Kilifi Kaunti, awaulize ni mikakati gani wako nayo na Serikali Kuu maana kuna uchunguzi. Kama hana *information* atwambie tumpatie hiyo *information* lakini si kuja hapa kwa sababu yeye ni *opposition* kule *Senate* aanze kuja kufanya hapa, *no!* Hatutakubali hiyo. Aje hapa atwambie ukweli siasa ni huko nje asubiri mwaka wa *2025* aje atwambie mambo ya siasa hapa. Asante.

The Temporary Speaker (Hon. Stephen): Asante, mheshimiwa Grace, kwa mchango wako. Mheshimiwa Rafiki, uwanja ni wako.

Hon. Rafiki: Asante, mheshimiwa Spika, kwa kunipa fursa hii. Kwanza, niseme mimi binafsi ninamheshimu sana *Senator* wa Kaunti ya *Kilifi*; ni kiongozi ninayemuenzi sana hasa katika chama changu. Lakini natafautiana naye kulingana na hotuba aliyoieleza hapa.

Mheshimiwa Spika, sisi ni watu wazima, na hii nchi tunajua inaendeshwaje. Mheshimiwa Seneta aliongea kwa machungu sana kuhusiana na zabuni za barabara akisema hizo *tender* zinapewa watu ambao si wenyeji na wanabeba pesa wanaenda wanatuachia barabara mbovu.

Mheshimiwa Spika, kigezo cha kwanza mtu kupewa kazi katika Kaunti ni awe ni mwenyeji. Si lazima *direct* awe na kitambulisho cha Kilifi, anaweza kuwa labda ni Hussein Abdallah Abdi wa Mandera lakini kampuni yake ina *single business permit* ya *County* ya *Kilifi*. *Qualification* ya kwanza ya kampuni kupewa kazi ni iwe na kibali cha kufanya biashara kwa hiyo Kaunti. Sasa Seneta akisema kuna kampuni za nje zinapewa kazi za watu ambao si wa Kilifi sijui alifanya utafiti wa kampuni ngapi ambazo aliona hazina vibali vya kufanya kazi kwa Kaunti yetu ya Kilifi.

Mheshimiwa Spika, swala la Shakahola, huyu Seneta alinishangaza sana. Hilo tukio la Shakahola ni la ukosefu wa usalama ambalo liko kwa Idara ya Serikali ya Kitaifa. Mheshimiwa Rais aliunda jopo la Wabunge la kuchunguza swala la Shakahola. Jopo hili laongozwa na mheshimiwa Danson Mungatana ambaye ni Seneta katika Seneti; Mungatana ni Seneta katika Jimbo letu la Pwani, makao makuu ya Serikali ya Kitaifa yako Nairobi na huyo Seneta Mungatana yuko Nairobi. Seneta anakuja hapa kutuzungumzia kuhusu miili ya Shakahola kuwa stima ya Kaunti inaenda ghali. Je, tukakate stima sisi? Mimi nafikiri kwa mtazamo wangu, haya amekuja yazungumza hapa alikuwa ni akayazungumze katika Bunge la Kitaifa, maana viongozi wahusika wote wako huko Nairobi. Sasa akija tulilia sisi kuhusu stima ya Kaunti iko ghali kwa sababu ya miili, tukaichukue tuitupe?

Swala la pili lililonishangaza mimi, nafikiri viongozi wanajisahau mapema sana. Aliongea kuhusu gharama ya maisha, kuwa Serikali Kuu inagandamiza wakenya kwa gharama ya maisha. Alitaja *Finance Bill* na *Housing Levy Bill.* Mheshimiwa Spika, nikukumbushe hivi, mheshimiwa Seneta wa Kilifi ni mmoja kati ya wale viongozi walishikwa wakiandamana kule Nairobi kwa kutetea gharama ya maisha, Spika wetu wa Bunge hili aliwekwa korokoroni zaidi ya wiki mbili akitetea gharama ya maisha. Cha kunishangaza mimi, baada ya Raisi amepeleka Mswada Bunge ili anayetaka kupinga Mswada huo waupinge na wale wakuupitisha waupitishe, Wabunge wa Kilifi wa Kitaifa wengine walikimbia, yeye akiwa mmoja wao Mswada ukapita. Sasa akija kulia hapa, Mswada unapigiwa kura Nairobi sasa sisi tufanyeje?

Seriously Bill ya Bunge juzi tu ilikuwa yapigiwa kura, mheshimiwa Spika wiki iliyopita. *List* ziko kwa magazeti za Wabunge wa Kitaifa waliokimbia kura hawakuipigia, wale walioitaka ikapita. Sasa akija tulilia sisi tufanyeje? Mimi kwa mtazamo wangu namaliza hivi, namheshimu sana, lakini ni muhimu pia akiongea, aongee vitu ambavyo vinahusiana na Kaunti ya Kilifi. Mimi nilikuwa natarajia mheshimiwa Seneta akisimama hapa atatwambia amepeleka Mswada huu wa Viwanda, Mswada huu wa Ajira, nimepeleka Mswada huu wa Ardhi, nimesukuma

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Serikali ya Kitaifa, kunakuja mradi huu na huu, yeye anakuja hapa kutukumbusha maswala ya Shakahola *seriously walahi* naona ajabu. Mimi namheshimu sana lakini hotuba yake sikubaliani nayo. Asante, mheshimiwa Spika.

The Temporary Speaker (Hon. Stephen): Asante, mheshimiwa Rafiki. Mheshimiwa Ngirani, baadaye tutakuja kwako.

Hon. Shehe: Asante, mheshimiwa Spika, kwa kunipatia hii nafasi. Sisi ni watu wa hekima sana, tumeketi katika hili Bunge na singependa tuchukuliwe kama kwamba vile mtu akija hapa achukulie kama kwamba twafanya nini. Sheria twazijua vilivyo na tunahakikisha kwamba baadhi ya wale ambao walitutuma hapa tunaangalia maslahi yao.

Mheshimiwa Spika, mwanzo alikuja kuchelewa. Yaani yeye hajui mambo ya wakati na ikawa ni hali ya shida ya wakati tuje ama atakuja saa ngapi? Yaani alitushika at *ransom.* Yeye hajali habari ya wakati, alikuja kuchelewa, sisi hatukulalamika tuliketi tukangojea.

Mheshimiwa Spika, katika mila zetu sisi huwa twasema cha mbachao usikiache lakini tuseme kwamba afadhali tuwe na heshima kwa kile tulicho nacho. Twamheshimu kweli huyu Seneta lakini aibu aliyoitoa hapa ni kitu cha kusikitisha. Tuna Gavana wetu hapa na watu wote ambao tuna waheshimu, ma Spika, tuna ma *County Clerk* na *some of the Senior Officials* wetu hapa lakini yeye hakujali hayo. Yeye alikuja na kurarua na kuonyesha kwamba wote hawajui kazi yeye ni kama amekuja kurekebisha. Sasa mimi wazo langu mheshimiwa Spika, ningeomba wale wageni ambao wanatoka katika hemaya hizi ambao wanalindwa na sheria ya kuwa anaweza kutoa *speech* kama hii, tuangalie zile *speech* zao ikiwa kwa mfano haziambatani na msimamo wetu haina haja kutupotezea wakati wetu. Huyu mheshimiwa tumheshimu lakini asitupotezee wakati wa upotovu.

(Applause)

Maanake ni kama tumekuja hapa twazungumza kitu ambacho sioni mwenzangu yeyote atasimama amuunge mkono. Na sio kwamba eti mimi nasimama nikiwa niko mrengo… mimi niko sawa sawa kwa sababu ukiwa wewe ni kiongozi katika *level* ya *Senate* ni lazima uwe unaweza kuheshimu hata na wenzako. Ikiwa Rais anatuheshimu na yeye kama Seneta anakuja kuchelewa, anakuja na matamshi anaanza ku *degrade* hata yale yaliyofanywa na Gavana ambaye wako chama kimoja na hata tusiangalie hapo.

Sasa ni kama kwamba tumekuwa hapa tunaongozwa na watu ambao hawaelewi kazi na yeye ndio amekuja kufanya kazi. Mimi yangu ni masikitiko kwa kuwa na kiongozi kama huyu ni kama kupoteza wakati; tunapoteza wakati kwa kweli. Ikiwa kwa mfano sisi tunasema yeye ndio kiongozi ambaye anaweza kutulinda maslahi yetu, ‘tumetupa mbao’. Yeye akiwa huko apige hizo *story* zake za masufuria na azungumze mambo mengi ambayo mimi siko na mambo ya kumwelewa mtu akiwa anaweza kuwa anaangalia wengine kwamba hawana maana. Yeye aende akapigane na huko Nairobi sisi nafikiria atuwache tufanye kazi yetu hapa. Asante.

The Temporary Speaker (Hon. Stephen): Asante sana mheshimiwa kwa hayo. Mheshimiwa Zia.

Hon. Zia: Asante sana, Bw. Spika, kwa kunipa nafasi hii. Mimi kwanza, nilichanguliwa na chama cha PAA (*Pamoja African Alliance*), Kenya kwanza. Seneta wetu ni mtu wa Azimio ODM (*Orange Democratic Movement*) na ndio maana wakati ule tulipokuwa tunapiga siasa tukawa tunasema kwamba huyu mzee aende kupumzika lakini kwa sababu ya wengi wape ni nchi ya demokrasia, wacha tu tukubali.

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Kulingana na hotuba yake ya wiki iliyopita imenifedhehesha sana, hasa kulingana na aliposema kwamba *Public Service Board* iko na ukabila; pengine hajafafanua vizuri.

Sisi tunakumbuka ya kwamba ilivunjwa ile ya kwanza ya *regime* ile ya kwanza alipokuwa Seneta wakati mheshimiwa Kingi akiwa Gavana. Tukaja tukaivunja mwaka jana; saa hii Bodi ni mpya na kwa kweli ni kwamba tayari imeajiri watu tisa peke yake na ni zile ngazi za juu; hawa *managers* katika hizi *parastatals* zetu ambazo ziko ndani ya hii Kilifi. Kwa sasa nataka niwaelezee wana Kilifi ya kwamba Bodi haijatangaza nafasi za kazi kwa wananchi wote wa Kilifi na karibuni itatangaza. Nikipata kuona kwamba huyu anasema kwamba iko na ukabila, kwanza sisi tuliipiga msasa vilivyo. Mimi pamoja na Kamati yangu na tukaleta hapa kwa Bunge na wakaipiga msasa vizuri na pia wakasema kwamba hii inafaa wachaguliwe Bodi.

Leo hii inasemekana kwamba kuna ukabila ambao unaendelea. Ukabila upi ambao unaendelea? Nafikiri Kiongozi wa Walio Wengi ndani ya Bunge ameonyesha wazi hata akataja makabila yaliyokuwa yamenaswa pengine awe yuko na mengine na ni kama kwamba anapiga siasa ya kivyake. Pengine kama anataka Ugavana aseme na kama anataka Ubunge na kama anataka kuwa *MCA (Member of County Assembly)* pia aseme.

Tukiangalia na nikinukuu vitu fulani fulani ambavyo amezungumzia, hasa swala la Shakahola. Mimi sijamuona Seneta wetu ambaye ni Madzayo kufika kule Shakahola na kuweka mkutano, kuzungumza na wananchi na kusema kwamba poleni wananchi wa huku Shakahola. Sijawahi kumwona, kama *area MCA*, kutoka wakati huo mpaka saa hii. Atuambie alikuwa yuko wapi na asisimame huko Nairobi na kusema kwamba; Shakahola! Shakahola! Na hajui Shakahola iko upande gani. Nasikitika sana, katika ile miili ambayo iko pale mimi nafuatilia vizuri sana, kwa hivyo kama hana taarifa aelezee ili tuweze kumjuza hizi habari.

Hapa Bungeni, nafikiri tulikuja tukazungumza na pia tukaleta *press* na hata pia walifika, Kiongozi wa Walio Wengi alifika katika hiyo sehemu na Gavana akafika hiyo sehemu lakini mbona yeye hajafika?

Pia amesema kwamba Wawakilishi wa Wadi wanatangamana na wananchi kule, ni ukweli lakini yeye hajazunguka katika hii Kilifi kutangamana na wananchi. Pengine sijui *Leader of Majority* kwa sababu yeye ni mtu wake katika chama anaweza kuwa pengine ashawekewa mkutano lakini kule kwangu mimi hajaweka. Wenzangu ambao wako hapa ndani katika Wadi zao alienda na kuweka mikutano huko akitangamana na wenzao. Tunapata majukumu makubwa kama waheshimiwa wa Bunge hili la Kilifi; tunapata shida sana kwa sababu huku kuna *gap* hakuna mtu ambaye anaweza kusaidiana na sisi katika nyanjani kule. Kila siku, Jumamosi na Jumapili, michango yote ni ya hawa Wabunge ambao wako huku chini wanaangaliwa. Uhusiano gani ambao yeye naye anauleta kwa wananchi kwa sababu wananchi wanapata shida katika zile sehemu zetu ambazo tunakaa.

Hajawahi kutuita, licha ya kuja hapa, lakini atuite kama Bunge aseme kwamba kando sasa munaenda vipi? Mko vipi? Nje ya hili Bunge atuite kando aseme kwamba ni changamoto gani ambazo mnazipata wabunge? Nimesimama hapa nikisikitika sana, nikisema kwamba hakuna shida haizuru lakini namshukuru kwa sababu ametuonyesha picha kamili kwamba alikuwa hafai kuwa Seneta wa hili Bunge. Asante sana.

Hon. Kubo: Asante sana, mheshimiwa Spika, kwa hii nafasi. Mimi niko na mambo matatu tu ambayo niliweza kusoma katika hotuba ile. Kusema kweli, mheshimiwa Spika, hotuba ile ya mheshimiwa Seneta sana sana alipokuwa akiongea hakugusia matatizo yetu sisi kama MCAs. Sisi tumekuwa na shida nyingi lakini yeye kama Seneta anajua zile shida tuko nazo.

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Tuseme kwamba angeweza kugusia shida kama zile tujue kwamba ako pamoja na sisi. Lakini hakugusia hata moja.

Jambo la pili; hotuba yake iliingilia sana upande wa Serikali Kuu na sisi kama UDA (*United Democratic Alliance*) hatukufurahia. Hata ile siku nakumbuka tu tumeanza kugusana gusana kidogo tutoke nje tuliona ametuingilia sana na hatukufurahia.

Jambo la mwisho kabisa, siku nyingine akija hapa, anafaa ajue kwamba yeye sio Seneta wa ODM, kwa wakati huu yeye ni Seneta wa watu wote wa Kilifi nzima, wa UDA, chama kile kingine kwa hivyo akija hapa aongee maswala ambayo yatakuwa yanatuhusu sisi sote. Sio kupangia sana upande wa ODM. Ningetaka kusema kwamba, Mheshimiwa Spika, siku nyingine akija na mambo kama hayo, sisi wa UDA tutatoka nje tumwache aendelee na wale wa ODM. Asante sana.

ADJOURNMENT

The Temporary Speaker (Hon. Stephen): Hon. Members, thank you for your good contributions towards the speech of our Senator. Now Hon. Members, there will be a resumption of debate in the afternoon sitting. We will accord a chance to the Members who have not spoken.

Therefore, there being no other business to transact, the House stands adjourned until 2:30 p.m. Let us keep time, please. Thank you.

The House rose at 10:13 a.m.

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*